BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

TNMC HABARI

Jarida la Mwezi

Toleo N0. 006

Machi , 2024

HALIUZWI

www.tnmc.go.tz @tnmchabari

# TNMC Yaadhimisha Miaka 71 Kwa kutoa Msaada wa Vifaa Tiba.

- *Yaelekea kutimiza Karne, Msajili abainisha Mafanikio.*
- *Wadau wa Afya wapongeza utendaji wa Baraza.*



MAADHIMISHO Miaka 71 Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania TNMC 1953 - 2024

# TIMU YA WAHARIRI

JARIDA MAALUMU BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

## MHARIRI MKUU

Bi.Agnes Mtawa

## MHARIRI

Mwakapiso Ndimmyake

## WARATIBU

Irene Chilewa na Rose Mhando

## MSANIFU JARIDA

Ezekiel M Nyalusi

P.O BOX1736 DODOMA
TEL.022-212133975 Fax.022-2133975 Mobile:0786785947

# Maadhimisho ya Miaka 71 ya TNMC kuelekea karne yafana Jijini Dodoma



*Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Agnes Mtawa, akikabidhi msaada wa vifaa tiba katika kituo cha Afya Makole Jijini Dodoma wakati wa Maadhimisho ya miaka 71 ya Baraza*

## Na Ndimmyake Mwakapiso

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania tarehe 19 Machi 2024, limeadhimisha miaka 71 tangu kuazishwa Mwaka 1953 kwa kufanya tukio la kijamii ambalo ni kutoa msaada kwa kukabidhi vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. 5,000,000 katika kituo cha Afya Makole kilichopo Jijini Dodoma.

Akizungumza mara baada ya kukabidhi vifaa tiba hivyo, Msajili wa Baraza Bi. Agnes Mtawa, amebainisha baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa na Baraza tangu mwaka 1953 kuwa ni pamoja na ukuaji wa Baraza kutoka kuwa Kitengo kidogo mpaka kufikia hadhi ya Taasisi chini ya Wizara ya Afya, yenye muundo wake wa kiutumishi ambao unakurugenzi mbili, vitengo sita na sehemu mbili.

Aidha idadi ya watumishi wa Baraza imeongezeka kutoka watumishi 2 mwaka 1992 hadi watumishi 35 mwaka 2024, idadi ya wauguzi na wakunga waliyosajiliwa na kuorodheshwa wenye viwango mbalimbali vya elimu imefikia 52,188, ambapo kati yao 17 ni Shahada ya Uzamivu, 382 ni Shahada ya uzamili, 5000, ni Shahada ya kwanza, 28,257 ni Stashahada wakati Astashahada wakiwa ni 18,532.

Mafanikio mengine ni pamoja na Ujenzi wa mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi orodha na taarifa za wauguzi na wakunga ambapo hapo awali taarifa za wauguzi na wakunga zilihifadhiwa kwenye kitabu cha nakala ngumu kilichofahamika kwa jina la Kalamazoo.

Ameyataja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na Ujenzi wa kituo cha Mafunzo katika Mji wa Kibaha sanjari na mradi unaoendelea wa ujenzi wa Ofisi kuu katika eneo la Medeli Jijini Dodoma.

***"Nitumie fursa hii pia kuwapongeza wauguzi na wakunga wote nchini kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuwahudumia wananchi wetu wenye changamoto mbalimbali za kiafya pia ninawakumbusha wauguzi na wakunga kote nchini, kuhakikisha mnatekeleza majukumu yenu kwa kuzingatia Utu na weledi huku mkijiepusha na ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma ili kuhakikisha wananchi wetu wanapata huduma bora zenye kiwango na salama"*** alisema Bi. Mtawa.

Akipokea vifaa tiba hivyo kaimu Mganga Mfawidhi wa kituo cha Afya Makole Dkt. Salma Gwasa, ameshukuru kwa Msaada wa vifaa vilivyotolewa na Baraza na kubainisha kuwa vifaa hivyo vitakuwa msaada mzuri kwa wao kama watoa huduma pamoja na wateja kwani vitasaidia kupunguza changamoto iliyopo katika utoaji huduma.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania lilianzishwa rasmi tarehe 19 Machi mwaka 1953 na sasa limefikisha miaka 71 huku likiwa na jukumu la kusimamia taaluma na wanataaluma wa kada za Uuguzi na Ukunga ili kuhakikisha jamii inapata huduma iliyobora na salama kutoka kwa wanataaluma hao.
Maadhimisho ya mawaka huu, yanachagizwa na kauli mbiu isemayo;
***"Wauguzi ni watu Maalum Kwa kazi Maalum"***

# Wauguzi Viongozi Wajadili Changamoto ya Wahitimu Wapya Kukosa Umahiri wa Kutosha



*Wauguzi viongozi katika mkutano wa mwaka - jijini Dodoma.*

**Na Ndimmyake Mwakapiso**

***"Ilituweze kuboresha huduma ya jamii inatakiwa kuwa na wauguzi na wakunga wenye umahiri na weledi wa kuhudumia jamii tukubali kuwa tunachangamoto ya wahitimu wanaotoka vyuoni kutokuwa na weledi wa kutosha, pia na walimu wasiyo na uzoefu wa kuweza kufundisha wanafunzi na kuwapa umahiri na weledi wa kutosha, haiwezekani mwalimu umetoka chuo ukaenda kufundisha wanafunzi wakati hujawahi kufanya kazi kwa vitendo"*** amesema Bi.Ziada sellah

Kauli hiyo imetolewa na Muuguzi Mkuu wa Serikali Bi. ziada Sellah, wakati wa mkutano wa mwaka wa wauguzi viongozi wa Mikoa, Halmashauri, Hospitali ya Taifa, Hospitali za Kanda, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali maalum, wauguzi wakufunzi kutoka Vyuo vikuu na Vyuo vya kati ulioandaliwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Muuguzi Mkuu ameendelea kusema, kuna umuhimu mkubwa mamlaka zinazohusika kuandaa wataalamu hawa ili kukaa pamoja na wadau wengine wa elimu kuona namna bora ya kuweka utaratibu mzuri wa utoaji mafunzo ya kada ya Uuguzi na Ukunga Tanzania.

***"Na ni ukweli usiopingika kwamba, tumekuwa tukipokea wahitimu ambao wamekuwa wakitupa mashaka makubwa, unakuta mwanafunzi anashindwa kufanya procedure ya msingi kabisa, ukweli inafikirisha, sisi kama walimu itabidi tutengeneze mjadala mwingine ambao wadau wote wa mafunzo tuweze kujadiliana haya, bado tunachangamoto na hii changamoto ni kubwa "*** Alisema Muuguzi Mkuu

Mkutano huu umefanyika Jijini Dodoma kuanzia 18 Machi 2024 hadi 23 Machi 2024 kwa lengo la kuwaleta pamoja Wauguzi viongozi kutoka ngazi zote za kutolea huduma za Afya nchini na wadau mbalimbali wa Afya kujadili na kupanga mikakati ya pamoja ya namna bora ya kuondoa malalamiko kwa wananchi kwa kuhakikisha huduma zinazojali utu, heshima, upendo na mawasiliano madhubuti baina ya mtoa huduma na mteja, pia kuweka mikakati ya kuimarisha usimamizi wa wanafunzi wauguzi katika maeneo ya kutolea huduma za afya.

Mkutano huu umebebwa na Kauli mbiu ***"Huduma sitaha na mawasiliano madhubuti ni wajibu wa kila mtoa huduma za Afya"***

# Wauguzi na Wakunga Viongozi Watakiwa Kushirikiana





*Dkt.Godwin Mollel akizungumza katika mkutano wa mwaka wa wauguzi viongozi - jijini Dodoma.*

***"Asilimia 60 ya watumishi wa sekta ya Afya nchini ni wauguzi na wakunga hivyo wanachangia ubora wa huduma zinazotolewa katika hospitali na vituo vya kutolea huduma za Afya"***
**amesema Dkt. Mollel**

## *Na Mwandishi Wetu*

Wauguzi na wakunga viongozi watakiwa kushirikiana katika usimamizi wa utoaji Huduma za Afya ili kuhakikisha huduma ya Afya inaboreshwa hapa nchini.

Rai hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Afya Mhe. Dkt. Godwin Mollel, wakati wa Mkutano wa mwaka wa wauguzi viongozi ulioandaliwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Naibu Waziri amesema asilimia 60 ya watumishi katika sekta ya Afya nchini wanatoka kada za Uuguzi na Ukunga hivyo kuchangia ubora wa huduma zinazotolewa katika Hospitali na Vituo vya kutolea huduma za Afya.

Pia ameongeza kuwa endapo wauguzi na wakunga watapata fursa ya kuingia ndani ya mfumo wa uongozi watasaidia kuhakikisha mambo yanaboreshwa kwenye kada ya Uuguzi na Ukunga.

Naye Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Agnes Mtawa, amewapongeza wauguzi vingozi kwa kuendelea kutoa ushirikiano mkubwa katika utendaji wa majukumu ya Baraza katika maeneo yao ya kazi.

***"Nitumie fulsa hii kuwapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya huko kwenye maeneo yenu ninyi ni wasaidizi wangu, fanyeni kazi kupunguza malalamiko ya wateja pia simamieni vyema wauguzi watarajali na wale wanao wabeza waleteni huku Barazani tutawashughulikia kwa mujibu wa Sheria"*** alisema Bi. Mtawa

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Usajili, Leseni na Maadili kutoka TNMC Bi. Jane Mazigo, amewataka Wauguzi viongozi kutoka ngazi zote za kutolea huduma za Afya nchini kusimamia vyema huduma za Afya sambamba na kuhakikisha huduma ya Uuguzi na Ukunga zinafuata Maadili, taratibu na miongozo ya huduma ya Afya.

Lengo la Mkutano huu ni kuwaleta pamoja Wauguzi viongozi kutoka ngazi zote za kutolea huduma za Afya chini na wadau mbalimbali wa Afya kujadili na kupanga mikakati ya pamoja ya namna bora ya kuondoa malalamiko kwa wananchi kwa kuhakikisha huduma zinazojali zinajali Utu, heshima, upendo na mawasiliano madhubuti baina ya mtoa huduma na mteja.




**Na Ezekiel Nyalusi**

**KWANINI SIKU HII NI MUHIMU?**
Kwa zaidi ya karne moja, watu kote Ulimwenguni wameadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake mnamo Machi 8.

**SWALI NI JE, KWANINI SIKU HII NI MUHIMU?**
Siku ya Kimataifa ya Wanawake ilianza vipi?
Siku ya Kimataifa ya Wanawake (IWD) ilitokana na harakati za wafanyakazi.
Mbegu hizo zilipandwa mwaka wa 1908, wakati wanawake 15,000 walipoandamana katika Jiji la New York wakidai kupunguzwa muda wa kufanya kazi, malipo bora na haki ya kupiga kura.
Mwaka mmoja baadaye, Chama cha Kisoshalisti cha Marekani kilitangaza Siku ya Kitaifa ya Wanawake ya kwanza.

Wazo la kulifanya kuwa tukio la kimataifa lilitoka kwa Clara Zetkin, mwanaharakati wa kikomunisti na mtetezi wa haki za wanawake, Mnamo 1910, alilizungumzia kwenye Mkutano wa Kimataifa wa Wanawake Wanaofanya Kazi huko Copenhagen nchini Denmark.
Pendekezo lake liliungwa mkono kwa kauli moja na wanawake 100 kutoka nchi 17 waliokuwa kwenye mkutano huo.
Siku ya kwanza ya Kimataifa ya Wanawake iliadhimishwa mnamo 1911, huko Austria, Denmark, Ujerumani na Uswizi.
Umoja wa Mataifa (UN) ulianza kuadhimisha tukio hilo mwaka 1975. Kaulimbiu ya kwanza iliyopitishwa na Umoja wa Mataifa (mwaka 1996) ilikuwa *"Kuadhimisha Yaliyopita, Kupanga Kwa Ajili Ya Baadaye"*.

### Kwa nini Siku ya Kimataifa ya Wanawake huadhimishwa tarehe 8 Machi?

Wazo la asili la Bi Zetkin la sherehe ya kimataifa halikuhusishwa na siku fulani.

Siku ya Kimataifa ya Wanaume hufanyika tarehe 19 Novemba tangu miaka ya 1990. Tukio hili halitambuliwi na Umoja wa Mataifa, lakini limeangaziwa katika zaidi ya nchi 80 duniani kote, ikiwa ni pamoja na Uingereza.

### Je, Siku ya Kimataifa ya Wanawake inaadhimishwaje duniani kote?

Siku ya Kimataifa ya Wanawake ni sikukuu ya kitaifa katika Nchi, nyingi nchini China, wanawake wengi hupewa mapumziko ya nusu siku ya kazi.
Maelfu ya matukio yanafanyika duniani kote, yakiwemo maandamano, mazungumzo, matamasha, maonesho na mijadala.

Nchini Italia, Siku ya Wanawake Duniani inaitwa Festa della Donna, na maua ya mimosa ni zawadi maarufu. Maua nchini Urusi kwa kawaida huongezeka maradufu karibu na Siku ya Kimataifa ya Wanawake.
Nchini Marekani, Machi ni Mwezi wa Historia ya Wanawake. Tangazo la rais linalotolewa kila mwaka linaheshimu mafanikio ya wanawake wa Marekani.





## Je, mada ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake 2024 nini?

Kaulimbiu ya Umoja wa Mataifa kwa mwaka 2024 ni *"Wekeza kwa wanawake: Ongeza kasi ya maendeleo"*, ambayo inalenga kuangazia umuhimu wa hatua za usawa wa kijinsia.

*"Migogoro na kupanda kwa bei kunaweza kusababisha 75% ya nchi kupunguza matumizi ya umma ifikapo 2025, na kuathiri vibaya wanawake na huduma zao muhimu,"* UN inaonya.

Tovuti ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake imechagua mada "Kuhamasisha Ushirikishwaji".

Inasema waandaaji na matukio yanalenga "kuvunja vikwazo, kupinga dhana potofu, na kuunda mazingira ambapo wanawake wote wanathaminiwa na kuheshimiwa."

## Je, kuna Siku ya Kimataifa ya Wanaume?

Siku ya Kimataifa ya Wanaume hufanyika tarehe 19 Novemba tangu miaka ya 1990.

Tukio hili halitambuliwi na Umoja wa Mataifa, lakini limeangaziwa katika zaidi ya nchi 80 duniani kote, ikiwa ni pamoja na Uingereza.

Siku hiyo inaangazia "thamani chanya ambayo wanaume huleta kwa ulimwengu, familia zao na jamii", kulingana na waandaaji.

Inalenga kuangazia mifano chanya ya kuigwa, kuongeza ufahamu wa ustawi wa wanaume na kuboresha mahusiano ya kijinsia.

Kwa miaka mingi, mcheshi Richard Herring alichangisha maelfu ya pauni kwa shirika la unyanyasaji la nyumbani la Refuge kila Siku ya Kimataifa ya Wanawake, kwa kujibu watu kwenye X, zamani Twitter, ambao walikuwa na hasira kuhusu ukosefu wa Siku ya Kimataifa ya Wanaume.

## Je, Wanawake wa Baraza la Uuguzi na ukunga Tanzania wameiadhimishaje iku hii hapa Tanzania?

Wanawake watumishi kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC), wameungana na wanawake wenzao kote Ulimwenguni katika kuiadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, ambapo Mkoani Dodoma Maadhimisho hayo yamefanyika Machi 8, 2024 Wilayani Chamwino katika viwanja vya Chinangali.

Aidha, Maadhimisho hayo yaliyobebwa na kauli mbiu isemayo, *"Wekeza kwa Wanawake kuharakisha Maendeleo ya Taifa na Ustawi wa Jamii"*

Ikumbukwe kuwa, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) ni Mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa kwa Mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 na Kanuni zake, kwa lengo la kusimamia wanataluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga, ili kuhakikisha jamii inapata Huduma za Afya zilizo Bora na Salama.

# Wauguzi Watarajali Wafundwa Kabla ya Kuanza Mafunzo kwa Vitendo



*Baadhi ya Wauguzi na wakunga watarajali Ngazi ya shahada ya kwanza wakifuatilia kwa makini maelekezo muhimu ya kitaaluma kabla ya kuanza mafunzo kwa vitendo katika kikao kilichoandaliwa na TNMC Jijini Dodoma*

***Na Ezekiel Nyalusi***

Wauguzi na wakunga watarajali zaidi ya 60 wa ngazi ya shahada ya kwanza wamepata maelekezo muhimu Jijini Dodoma kutoka kwa Baraza la Uuguzi na Ukunga kabla ya kuanza mafunzo kazini katika Hospitali mbalimbali hapa nchini.

Akifungua mafunzo elekezi msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Agnes Mtawa, amewataka watarajali hao kwenda kujifunza kwa kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa ikiwa ni pamoja na kuripoti katika kituo cha mafunzo kwa mujibu wa tarehe zilizoainishwa katika burua ya kupangiwa kituo, kufuata na kuzingatia ratiba na taratibu za kazi katika kituo cha mafunzo, kutoa taarifa kwa msimamizi wa mafunzo endapo kutakuwa na dharura yoyote ya kutofika kituoni, kushiriki mafunzo kwa vitendo, kufuata taratibu, kanuni, Sheria na sera za kituo

Katika hatua nyingine Bi. Mtawa, amewataka wauguzi wote nchini kutenga muda wa kupitia Sheria ya Uuguzi na Ukunga ili kujua majukumu na utendaji kazi wa Baraza.

***"Niwatake wauguzi wote kutenga muda wa kujifuza kwa kina yapi majukumu ya Baraza, kwani wauguzi wengi wanashindwa kulijua hili ambalo lipo wazi kabisa na lipo kisheria, hivyo someni Sheria iliyopo kwenye Tovuti ya Baraza pamoja na miongozo yake"*** amesema Bi.Mtawa.

Naye Mkurugenzi wa usajili na maadili Bi.Jane Mzigo, amewataka wataraji hao kuzingatia maadili pamoja na kuwatia moyo wanapokwenda kuihudumia jamii.

***"Muipende taaluma kafanyeni kazi kwa uadilifu, mimi natamani tungeongozana tukafanye kwa pamoja, mkazingatie usafi na kuvaa vizuri ili kujipambanua kuwa wewe ni Muuguzi unayetegemewa"*** amesema Bi.Mazigo

Kwa upande wake Mwanasheria wa Baraza Bw. Ayubu Lazaro, amewakumbusha kuwa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ilitungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010 ambapo Baraza linawajibu wa kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo.

# Katibu Mkuu Dr. John Jingu: Toeni Huduma Kwa Kuzingatia Lugha Zenye Staha





*Katibu Mkuu Dkt. John Jingu akizungumza na watumishi wa Afya Hospitali ya Rufaa ya Sekou Toure na Hospitali ya Kanda Bugando*

## *"Serikali imewekeza kwa asilimia kubwa katika sekta ya Afya ikiwemo miundombinu, vifaa tiba na dawa"* - Dkt. Jingu

*Na Mwandishi wetu*

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu, amewataka wahudumu wa Afya nchini kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kuzingatia lugha zenye staha na kutoa huduma stahiki kwa wagonjwa.

Dkt. Jingu ameyasema hayo wakati akiongea na watumishi wa sekta ya Afya mkoani wa Mwanza baada ya kutembelea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa huo Sekou Toure na Hospitali ya Kanda Bugando akiwa ameongozana na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu.

Dkt. Jingu amesema kazi ya utumishi wa Afya ni kazi maalum ambayo inalengwa kwa watu maalum hivyo kila mtu awajibike kutekeleza kazi zake kwa ufanisi hali itakayowezesha kutaboresha huduma za Afya nchini

***"Serikali imewekeza kwa asilimia kubwa katika sekta ya Afya ikiwemo miundombinu, vifaa tiba na dawa hivi vyote havina tija kama hatutokua na huduma nzuri kwa wateja, hivyo tutumie lugha nzuri na yenye staha ikiwa ni Pamoja na kutoa huduma stahiki kwa wagonjwa"*** Amesema Dkt. Jingu

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu amewaasa watumishi hao kuendelea kujali na kuthamini huduma bora kwa wananchi huku akiwatia moyo watumishi kuendelea kutoa huduma bora ndani ya jamii.

Prof. Nagu, amewapongeza watumishi hao kwa juhudi kubwa ya kuwajali na kuwathamini wagonjwa kwani kazi ya kuwahudumia wagonjwa ni Kazi maalum kwa watu maalum.

Akizungumza kwa niaba ya Watumishi Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Sekou Toure Dkt. Bahati Msaki, amemshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu, Pamoja na Mganga mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu, kwa kuwasihi na kuwapongeza watumishi hao Pamoja na kuahidi kuendelea kufanya kazi kwa juhudi ili kuboresha huduma za Afya kwa jamii.

# Mkurugenzi TAMISEMI Alipongeza Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania kwa Uwajibikaji





*Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Lishena Ustawi wa jamii OR-TAMISEMI Dkt. Mfaume akizungumza katika Mkutano wa mwaka wa wauguzi viongozi - Jijini Dodoma.*

## Na Mwandishi Wetu

Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Lishena Ustawi wa jamii OR-TAMISEMI Dkt. Rashid Mfaume, amelipongeza Baraza Uuguzi na Ukunga kuilinda Afya ya jamii kwa kuisimamia vyema Taaluma ya Uuguzi na Ukunga nchini.

Pongezi hizo amezitoa wakati wa mkutano wa mwaka wa wauguzi viongozi wa mikoa, Halmashauri, Hospitali ya Taifa, Hospitali za Kanda, Hospitali za Rufaa za mikoa, Hospitali maalum, wauguzi wakufunzi kutoka Vyuo vikuu na Vyuo vya kati ulioandaliwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

***"Nimefurahishwa sana na utendaji wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania pia nawapongeza kwa kuadhimisha ya miaka 71 tangu kuazishwa kwa Baraza lakini pia, nikupongeze Msajili wa Baraza Bi.Agnes Mtawa, kwa usimamizi mzuri wa kulinda maadili ya kitaaluma hongereni sana Baraza"*** amesema Dkt.Mfaume.

Ameongeza kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, anawadai wauguzi na wakunga, kwani yeye

> ***"Nikupongeze Msajili wa Baraza Bi.Agnes Mtawa, kwa usimamizi mzuri wa kulinda Maadili ya kitaaluma hongereni sana Baraza"***
>
> *- amesema Dkt. Rashid Mfaume*

amekwishaboresha mazingira ya kutendea kazi kwa ngazi zote hivyo, wauguzi na wakunga wanawajibu wa kutimiza majukumu yao na kusimamia vyema huduma za Uuguzi na Ukunga.

Naye Rais wa chama cha Uuguzi na Ukunga Tanzania Bwana Alexanda Balulya, amewataka wauguzi na wakunga kuachana na ubaguzi wa kitaaluma ili kufika mbali katika utendaji

***"Ubaguzi wakitaaluma hautakiwi katika utendaji kazi, tutunziane heshima na mapungufu ya kitaaluma huku tukiitatua migogoro midogo midogo katika tasnia yetu tusikimbilie kwenye vyombo vya habari"*** amesema Bwana Balulya.

# TANZIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga limepokea kwa masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele za haki Mwezi Machi mwaka 2024, baada ya kumaliza kazi yao hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao mahali pema Peponi AMINA.



**JINA: HADIJA ANTONY**
**KITUO :** Kiomboi district Hospital
**WILAYA :** Iramba DC
**MKOA :** Singida



**JINA: ESTER PAULO GOLIAMA**
**KITUO :** Liwihi Dispensary
**WILAYA :** Mbinga DC
**MKOA :** Ruvuma



**JINA: SHIRINI SHARIF**
**KITUO :** Ocean road cancer institute
**WILAYA :** Ilala MC
**MKOA :** Dar es salaam



**JINA: TATU BUKANU**
**KITUO :** Ngudu District Hospital
**WILAYA :** Kwimba DC
**MKOA :** Mwanza



**JINA: ELIZABETH LUMATO**
**KITUO :** Nyampande Dispensary
**WILAYA :** Sengerema DC
**MKOA :** Mwanza

JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA
TANZANIA TOLEO NO 05

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu:0737-96-26-91**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA